

Virusi vya Corona Ukweli na Uongo:

Kuna uongo MWINGI unaozunguka kuhusu virusi vya Corona kupitia maneno ya mdomo na mtandao wa kijamii. Tutashughulikia BAADHI ya uongo hapa chini, lakini ni MUHIMU SANA kutosambaza habari potofu. Kama ilivyotajwa hapo juu, iACT itaendelea kuwasiliana na jamii yako kuhusu sasisho halisi kuhusu virusi vya Corona. Ukitaka habari zaidi, unaweza kutembelea tovuti maarufu kama Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa ([CDC.gov](https://www.cdc.gov)) na Shirika la Afya Duniani ([WHO.int](https://www.who.int)). Unaweza pia kuwasiliana na wafanyakazi wa iACT katika jamii yako kuhusu maswali yanayohusu virusi vya Corona. Wafanyakazi wa iACT walioko Marekani watawasiliana na wafanyakazi katika jamii yako.

● **Uongo:** Virusi vya Corona haviwezi kuambukizwa katika maeneo yenye hali ya hewa ya joto na yenye unyevu.

Ukweli: Virusi vya Corona vinaweza kuenea MAENEO YOTE, ikiwa ni pamoja na maeneo yenye hali ya hewa ya joto na yenye unyevu.

● **Uongo:** Kuoga maji ya moto kunaweza kuzuia Virusi vya Corona.

Ukweli: Kuoga maji ya moto hakutakuinga kupata virusi vya Corona. Kwa hakika, kuoga maji ya moto sana kunaweza kukudhuru, kwani kunaweza kukuchoma.

● **Uongo:** Virusi vya Corona vinaweza kuenezwa kupitia kuumwa na mbu.

Ukweli: Hapana, kufikia sasa hakuna taarifa wala ushahidi unaoashiria kwamba Virusi vya corona vinaweza kuenezwa na mbu.

● **Uongo:** Kujinyunyizia kileo, klorini, au dawa ya kuondo madoa mwilini kutaua Virusi vya Corona.

Ukweli: Hapana. Havitaviua virusi ambavyo tayari vimeingia ndani ya mwili wako. Kunyunyiza vitu kama hivyo kunaweza kuleta madhara kwa mavazi na nembreni laini (kama vile, macho, mdomo).

● **Uongo:** Chanjo dhidi ya nimonia inaweza kukulinda dhidi ya virusi vipya vya Corona.

Ukweli: Chanjo dhidi ya nimonia haitoi kinga yoyote dhidi ya Virusi vya Corona. Virusi hivi ni vipya na tofauti sana kiasi kwamba vinahitaji chanjo vyao vyenyewe na watafiti wanaendelea kuunda chanjo.

● **Uongo:** Hali ya hewa ya baridi na theluji vinaweza kuua virusi vipya vya Corona

Ukweli: Hapana, hakuna sababu ya kuamini kwamba hali ya hewa ya baridi inaweza kuua virusi vya Corona.

● **Uongo:** Kula/kunywa _____ kunaweza kukinga dhidi ya virusi vya Corona.

Ukweli: Hakuna ushahidi kutoka kwenye mlipuko wa sasa kwamba kula/kunywa baadhi ya vitu kumewakinga watu dhidi ya virusi vya Corona.

● **Uongo:** Ni wazee tu wenye umri zaidi ya miaka 60 wanaoweza kuambukizwa virusi vya Corona.

Ukweli: Hapana, watu wenye UMRI WOWOTE wanaweza kuambukizwa virusi vya Corona (Tafadhali tazama sehemu ya "Dalili").

● **Uongo:** Dawa za antibiotiki zinafaa kutumika kukinga na kutibu virusi vya Corona.

Ukweli: Hapana, antibiotiki hazifanyi kazi dhidi ya virusi, ni dhidi ya bakteria tu.

● **Uongo:** Zipo dawa maalumu za kukinga na kutibu virusi vya Corona.

Ukweli: Kufikia sasa, hakuna dawa mahususi ya kukinga na kutibu virusi vya Corona.

● **Uongo:** Virusi vya Corona vitapotelea mbali miezi ya msimu wa joto.

Uongo: Hapana, mlipuko iliyopita ya dunia nzima ya ugonjwa haukuendana na hali ya hewa na pia wakati Nusu ya Dunia iliyo Kaskazini ikiingia majira ya joto, majira ya baridi yataanza katika Nusu ya Dunia iliyo Kusini. Virusi ni vya kudunia.

● **Uongo:** Kama unaweza kujizuia bila kuvuta pumzi kwa sekunde kumi bila tabu, basi huna virusi vya Corona.

Ukweli: Hapana, wengi wa wagonjwa vijana walio na virusi vya Corona wanaweza kujizuia bila kuvuta pumzi kwa muda mrefu zaidi ya sekunde 10. Wazee wengi wasio na virusi hawataweza kufanya hivyo.

● **Uongo:** Virusi vya Corona vinaishi kooni. Kunywa maji mengi ili virusi visombwe kwenda tumboni ambako asidi itaviua.

Uongo: Virusi vya Corona vinaweza kuingia mwilini kupitia kooni, lakini hujipenyeza kuingia ndani ya seli za mtu. Huwezi kuvisomba na maji.

● **Uongo:** Sanitaiza ni bora kuliko sabuni na maji.

Ukweli: Hapana, sabuni na maji hua na kuviosha mbali virusi kutoka kwenye ngozi (haviwezi kujipenyeza kwenye seli zetu za ngozi). Pia husafisha uchafu wa mchanga unaonekana. Sanitaiza ni muhimu kutumika pale sabuni na maji havipatikani.

Endeleza na usambaze nakala hii ya Ukweli ya iACT na usisambaze taarifa zisizo kweli!